

Jina..... Nampari yako...../.....
Shule..... Tarehe

Sahihi ya Mtahiniwa.....

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

(FASIHI)

JULAI / AGOSTI - 2012

MUDA: SAA 2 ½

TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA ZA BORABU NA MASABA KASKAZINI- 2012
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari

MAAGIZO

1. Jibu maswali MANNE pekee
2. Swalii la kwanza ni la LAZIMA
3. Chagua maswali mengine matatu kutoka sehemu zilizosalia
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
5. Kila swali lina alama 20

Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa

Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mitihani zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo

For More Free KCSE past papers visit www.freerksepastpapers.com

A) MAYAI WAZIRI WA MARADHI

1. Huku ukirejelea hadithi zozote kumi thibitisha ukweli kuwa “Ibilisi wa mtu ni mtu”
(Alama 20)
2. “Hakupata kuchangamka katika nyumba lie, mpakaMashaka. Na sasa maadamu anaondoka”
 - a) Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)
 - b) Taja sifa nne za aliyekosa kuchangamka mpaka..... (Alama 2)
 - c) Fafanua kwa kutumia wahusika wanne kama vietelezo vya mwanga wa kumaliza dhiki za Utengano. (Atama 8)
 - d) Angazia mashaka manne yaliyomsibu anayeondoka alipoondoka. (Atama 4)
 - e) Badili ya tukio hili, taja mengine mawili yaliyobadili mkondo wa maisha ya baadhi ya wahusika.
au
(Alama 2)
3. Thibitisha kauli kwamba uchochezi ndio umefanikisha Riwaya ya Utengano. (Alama 20)

C) KIFO KISIMANI:Kithaka wa Mberia

4. “Hivi punde utakuwa na kazi. Na usiifanye nusunusu”
 - a) Fafanua muktadha wa dondo hili. (Alama 4)
 - b) Eleza sifa mbili za mzungumzaji na umuhimu wake. (Atama 4)
 - c) Hatima ya msemaji ni chanzo cha lengo Ia apokeaye tendo. Thibitisha. (ALama 8)
 - d) Kumetumika mbinu gani ya uandishi katika dondo hili? Taja na kueleza. (Atama 4)

D) FASIHI SIMULIZI

5. a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo. (Alama 5)
 - i) Rara
 - ii) Methali
 - iii) Lakabu
 - iv) Ngomezi
 - v) Ushairi simulizi
- b) Vianzio vya ngano vina majukumu mengi. Taja matano. (Alama 5)
- c) Taja methali mbilimbili ambazo kwazo istilahi zifuatazo zinajitokeza. (Alama 4)

- i) Istiari
 - ii) Tashbihi
 - iii) Tashhisi
- d) Ili mtampaji afanikishe utambaji wake, anahitaji mazingira yapi? (Alama 3)
- e) Eleza njia zozote tatu za ukusanyaji wa fasihi simulizi. (Alama 3)

E) USHAIRI

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata

1

Mvuwa iliyonyesha, ya maradi na ngurumo

Kutwa na kucha kukesha, kunyesha pasi kipimo

Haikuwanufaisha, wenye kazi za vihmo

Wenye kazi za vilimo, walifikwa na hasara

2

Mimeya waloipanda, ilitekukatekuka

Kazi ngumu walotenda, yote ikaharibika

Hawakuvuna matunda, waliyo wakiyataka

Waliyo wakiyataka, yakawa ya mbali nao

3

Wenye kuicha mvuwa, isiwatose mwilini

Baadhi yao wakawa, wakimbiliya penuni

Wengine hawakutuwa, hadi mwao majumbani

Hadi mwao majumbani, na kukomeya milango

4

Wenzangu dhihaka kando, nisemayo ni yakini

llibwaga kubwa shindo, mvuwa hiyójamani

Na mijaji kwa mikondo, yakawa barabarani

Yakawa barabarani, mvuwa kwisha kunyesha

5

Kunyesha iliposiya, kukatapakaa tope

Zilijaa'kila ndiya, isibakiye nyeupe

Ukawa mwingi udhiya, pa kupita zisitup
Pa kupita zisitupe, kwa ndiya kukosekanza

6

Japo hivyo zilikuwa, ndiya hazipitike
Bali mimi haamuwa, kwenenda japo kwa dhiki
Kumbe vile nitakuwa, ni mfano wa samaki
Ni mfano wa samaki, kuiendeya ndowana

7

Zikanibwaga telezi, sikujuwa kuzendeya
Ningekwenda kwa henezi, yasingenifika haya
Lakini tena siwezi, wendo huo kutumiya
Sitawata kutembeya, ila tabadili mwendo

Maswali

- a) Pendekeza kichwa mwafaka kwa shairi ulilosoma. (Alama 1)
- b) Kando na kuwa tarbia, pendekeza bahari zingine zozote tatu. (Alama 3)
- c) Fafanua maudhui yaliyojitokeza katika shairi. (Alama 4)
- d) Uhuru wa kishairi umetumika vipi katika shairi hili ? (Alama 4)
- e) Andika ubeti wa sita katika lugha nathan. (Alama 4)
- f) Taja na ueleze mbinu zozote mbili za lugha katika shairi hili. (Alama 2)
- g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kwa mujibu wa shairi. (Alama 2)
 - i) Kuicha
 - ii) Henezi

7.

Nilipoanza safari, ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa an, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

Njaa ikawa thibiti, na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati, tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti, dhila na mingi mikiki

Tulijizatiti

Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari, utumwa hatuutaki
Kuwa mbeie\’a safari, juhudri iliyobki
Tulijizatiti

Ile ilikuwa ndoto, mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto,sahili ‘mekuwa dhiki
Wagombania kipato, utashi haukatiki
Na kutabakari

Msafara ukasita, kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatupita, miima haupandiki
Basi sote ‘kajipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

Tukiwa migongo wazi, tukainama kwa shaki
Tukawa ‘chia ukwezi, kileleni wadiriki
Wakapanda bila kazi, kuteremsha miliki
Wakaitapia

Wakafikia makazi, yapumbao na ashiki
Huko wakajibarizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema mate, kwea umati halaiki
imezima nia yote, kiza hakitakasiki
Mbeie ya safari

Maswali

- a) Pendekeza mada moja kuu inayoafiki ujumbe wa shairi. (Alama 2)

- b) Shairi hill ni la bahari gani ? Taja na njeleze zozote tatu. (Alama 3)
- c) Taja matatizo ya watu kulingana na shairi. (Alama 3)
- d) Wanaohusishwa na shairi hill wana sifa gani? (Alama 4)
- e) Ni upi muundo wa shairi hili? (Alama 4)
- f) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (Alama 4)

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com